

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA TISA

18 APRILI, 2023



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

KIKAO CHA TISA – TAREHE 18 APRILI, 2023

I. DUA:

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (UTUMISHI NA UTAWALA BORA):

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

II. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

108. MHESHIMIWA EMMANUEL LEKISHON SHANGAI (NGORONGORO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Mto Piyaya Kata ya Piyaya na Mto Juhe Kata ya Samunge.

**109. MHESHIMIWA CONSTANTINE JOHN
KANYASU (GEITA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za ukarabati wa Madarasa, Mabweni na Usafiri katika Shule ya Sekondari ya Geita.

**110. MHESHIMIWA ANTON ALBERT
MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini ujenzi wa soko la Kimataifa la Ndizi katika Kata ya Kiwira utaanza.

**111. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA
(BUYUNGU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni Wazee wangapi wamepewa Bima ya Wazee na waliobaki ni lini watapewa Bima hizo Wilayani Kakonko.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

112. MHESHIMIWA ALLY JUMA MAKOA (KONDOA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini barabara ya Km 0.8 kutoka Benki ya NMB hadi *National Milling* Kondoa Mjini itajengwa kwa kiwango cha lami.

113. MHESHIMIWA DANIEL BARAN SILLO (BABATI VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa barabara ya Mbuyu wa Mjerumani hadi Mbulu.

114. MHESHIMIWA AHMED ALLY SALUM (SOLWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa barabara ya Manangwa, Mwakitolyo hadi Bulige utanza.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

115. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini mpaka wa Hifadhi ya Ugalla utarekebisha ili kurejesha kwa Wananchi eneo walilokuwa wanatumia kwa ufugaji.

WIZARA YA KILIMO:

116. MHESHIMIWA BERNADETHA KASABAGO MUSHASHU (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itatafuta Soko la uhakika la Zao la Vanilla.

WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:

117. MHESHIMIWA NAGHENJWA LIVINGSTONE KABOYOKA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini Serikali itaweka katazo la Kisheria la kuswaga Mifugo ili kuzuia uharibifu wa mazingira.

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

**118. MHESHIMIWA BAHATI KENETH NDINGO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utamaduni,
Sanaa na Michezo:-

Je, kuna mkakati gani wa kuhakikisha Jamii
inarudi katika maadili mema kutokana na
ongezeko la mmomonyoko wa maadili.

WIZARA YA AFYA:

**119. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON
MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini changamoto ya ukosefu wa Madaktari
Bingwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kitete
itatatuliwa.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

**120. MHESHIMIWA AGNES ELIAS HOKORORO
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na
Sheria:-

Je, kuna mpango gani wa kubadilisha Sheria ya mirathi ya Kiserikali ya Mwaka 1925 na Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:

121. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuamua kuwa Wasichana wasiolewe chini ya miaka 18.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

122. MHESHIMIWA NG'WASI DAMAS KAMANI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

Je, lini Serikali itaona haja ya kuondoa malipo ya Kodi kwa Wajasiriamali kabla ya kuanza rasmi kufanya biashara.

III. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
18 APRILI, 2023**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**

